



# TUZO ya AZAKi Bora 2007

Kwa Asasi za Kiraia zilizofanya Vizuri Zaidi Mwaka 2007



## Wito wa Kushiriki

### Kuhusu Tuzo

The Foundation for Civil Society inayo furaha kutangaza Tuzo ya kwanza ya AZAKi Bora Tanzania “Tanzania CSO Excellence Award” 2007. Tuzo hii itakayokuwa ikitolewa kila mwaka ina lengo la kuzitambua AZAKi zilizofanya shughuli zake kwa ufanisi na ubora wa kiwango cha juu katika mwaka husika.

Tuzo hii inatoa fursa ya:

- kutambua na kuenzi mchango wa AZAKi katika harakati za maendeleo nchini
- Kukuza ufahamu wa jamii kuhusu mchango wa AZAKi katika kuleta maendeleo na kupunguza umasikini nchini
- Kutoa fursa kwa asasi zingine kujifunza ili kuboresha zaidi utendaji wao.

### Nani anaweza Kushiriki

- Tuzo hii itahusisha washindani ambao ni AZAKi<sup>1</sup> zilizosajiliwa katika ngazi mbalimbali na zinazofanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar)
- AZAKi ziwe za hapa nchini (siyo za kimataifa)
- Washindani wawe wamefanya jambo kubwa na la maana lililoleta mabadiliko makubwa na endelevu kwa jamii kwa mwaka husika
- Maombi ya ushiriki yawe katika lugha ya Kiswahili.

### Vigezo vya Ushindani

Habari zinazotakiwa kutolewa na AZAKi zijumuishe maelezo yanayohusu maeneo yafuatayo:

- I. Mabadiliko yaliyotokea kwa jamii kutokana na kazi zenu: Washindani waeleze bayana matokeo na faida za kiwango cha juu ambazo zimepatikana kwa jamii kutokana na kazi za asasi, ubunifu wake na umahiri katika utekelezaji wa mradi husika.
- II. Ushiriki na ushirikishwaji wa walengwa na uendelevu wa mabadiliko yaliyotokea: Washindani waonyeshe kwa mifano dhahiri kiwango cha juu cha ushirikishwaji wa walengwa katika kubuni, kutekeleza na kupima matokeo ya mradi ulioleta mabadiliko makubwa katika jamii. Pia waeleze mikakati ya uendelevu wake.



	<p>III. Kupanua mitandao na kujenga umoja miongoni mwa AZAKi, serikali na sekta binafsi: Washindani waelezee kwa mifano dhahiri kazi za kiwango cha ubora wa kipekee ambazo asasi imefanya katika kukuza mitandao na ushirikiano miongoni mwa AZAKi sambamba na juhudi zake za makusudi za kuimarisha ubia kati yake na sekta binafsi, serikali, wabunge na asasi za kiraia.</p> <p>IV. Utawala Bora na Uwajibikaji ndani na Nje ya Asasi: Washindani watoe maelezo na mifano dhahiri ya mafanikio yao kuhusiana na ubora wa muundo wa asasi, mfumo wa utawala na uongozi unavyofanyakazi, uwepo wa miongozo ya fedha na uwajibikaji katika udhibiti wa fedha, haki na miongozo kwa viongozi, watendaji na wafanyakazi na watu wa kujitolea katika asasi husika.</p> <p>V. Uwazi: Washindani waonyesha kwa mifano dhahiri jinsi asasi inavyotilia maanani uwajibikaji, uwazi na uadilifu, utoaji taarifa za miradi na fedha kwa mamlaka husika, walengwa na wananchi kwa ujumla.</p>
<p><i>Mchakato wa Kuchagua AZAKi Bora 2007</i></p>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tuzo hiyo itakuwa na wawakilishi wa kanda<sup>2</sup> ili kuhakikisha mikoa yote nchini ina fursa ya kushiriki katika mchakato huu.</li> <li>• Maelezo ya ziada kutoka upande mwingine (kama vile viongozi wa kiserikali au kidini) yatatiliwa maanani katika mchakato wa kuchagua mshindi.</li> <li>• Tarehe ya mwisho ya kuleta maombi ni 15 Januari, 2008.</li> <li>• Mshindi atachaguliwa na jopo huru la majaji. Mshindi wa kwanza hadi wa tatu kutoka kila kanda atazawadiwa. Mshindi wa kwanza kutoka kila kanda atashiriki katika kugombea zawadi ya kitaifa.</li> </ul>



<i>Jinsi ya kuleta fomu ya maombi</i>	<p>Mshiriki atume fomu yake iliyojazwa vizuri kwa The Foundation for Civil Society pamoja na:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Habari za ziada katika vipeperushi, vipande vya magazeti (newspaper cuttings) kuhusiana na AZAKi na mafanikio yake.</li> <li>• Barua kutoka viongozi wa serikali au dini kumuunga mkono mshindani katika kugombea zawadi.</li> </ul>
<i>Zawadi</i>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Washindi wa Kwanza hadi wa Tatu Kitaifa watapewa zawadi za Fedha taslimu, Ngao na Vyeti.</li> <li>• Washindi wa kwanza na wa pili wa kila kanda pia watazawadiwa.</li> </ul>
<i>Fomu ya Maombi</i>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Fomu ya maombi na habari nyingine zaidi kuhusu Tuzo ya AZAKi 2007 zinapatikana kwenye tovuti (<a href="http://www.thefoundation-tz.org">www.thefoundation-tz.org</a>) au kutoka: The Foundation for Civil Society Haidery Plaza, Ghorofa ya tano, Kona ya Mitaa ya Upanga/Kisutu, S.L.P. 7192, Dar es Salaam, Barua Pepe: <a href="mailto:maendeleo@thefoundation-tz.org">maendeleo@thefoundation-tz.org</a> Tovuti: <a href="http://www.thefoundation-tz.org">www.thefoundation-tz.org</a></li> </ul>
<i>Tarehe ya Mwisho</i>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tarehe ya mwisho ya kuleta maombi ni 15 Januari, 2008.</li> </ul>

- 1 *Asasi za Kiraia (AZAKi) ni taasisi zinazofanya kazi nje ya familia, sekta ya biashara na serikali kutetea maslahi ya jamii/umma. AZAKi zinajumuisha Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE), Vikundi vya Kijamii (CBOs), Vyama vya Wanahabari, Vyama vya Wafanyakazi, Asasi za Kidini, Vyama vya Msingi vya Ushirika.*
- 2 *Kutakuwa na kanda 8 za mchakato wa kuwapata washindi. Kanda hizo ni Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam na Pwani), Kanda ya Magharibi (Kigoma, Tabora), Kanda ya Kaskazini (Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga), Kanda ya Njanda za Juu Kusini (Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma), Kanda ya Kusini (Mtwara, Lindi), Kanda ya Kati (Dodoma, Morogoro, Singida), Kanda ya Zima (Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera) na Kanda ya Zanzibar (Unguja na Pemba)*

